**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI WA KAHAMA**

SHULE YA SEKONDARI KINAGA,
S.L.P 413,
**KAHAMA.**

KUMB.NA. KNSS/J.L10
MZAZI/MLEZI WA …………………………………..

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KINAGA MWAKA 2021.**

1. Ninayofuraha kubwa kukuarika kuwa mwanao ………………………… amechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Kinaga, shule hii ni ya kutwa iliyopo kata ya Kinaga kwa masomo ya Sekondari kidato cha kwanza mwaka 2021 hivyo shule itafunguliwa kwa muhula wa kwanza mnamo tarehe ……………..
2. Tafadhari mara baada ya kuipata na kuisoma barua hii unatakiwa kumkamilishia mwanao mahitaji yote yaliyo orodheshwa ili kumwezesha akubalike shuleni katika muda uliopangwa.
3. Mwanafunzi hatapokelewa shuleni baada ya wiki mbili tangu shule ifunguliwe, ambapo nafasi yake itachukuliwa na wale wa akiba kwa maamuzi ya katibu tawala na si vizuri kusukumwa.

**MAHITAJI YA SHULE**

4. Mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni na vifaa vifuatavyo:-

**A) VIFAA**

i. Madaftari makubwa kumi na moja (11) counter book Q2
ii. Mkebe (mathematical set) moja 1
iii. Kalamu za wino wa bluu mbili (2)
iv. Penseli moja (1)
v. Kifutio kimoja (rubber)
vi. Rula yenye sm 30 moja
vii. Kamusi ya kiingereza (dictionary) moja (1)
viii. Begi dogo la kubebea madaftari
ix. Karatasi za kujibia mitihani.

**B) SARE ZA SHULE (SCHOOL UNIFORM)**

- **WAVULA**
  - Suruali mbili 2 za shule rangi ya kijivu
  - Viatu vya ngozi nyeusi vya kufunika mguu, visiwe na visigino virefu na si mabuti (Jozi mbili)
  - Mashati meupe mikono mifupi ya heshima yanayochomekwa kwenye suruali 2
  - Soksi nyeupe jozi mbili
  - Mkanda wa ngozi mweusi wa heshima usiwe na picha au mchoro wa Aina yoyote
  - Tracksout ya michezo rangi ya Blue

- **WASICHANA**
  - Sketi mbili 2 za heshima ziwe ndefu zinazofunika miguu rangi ya kijivu
  - Mashati meupe mawili 2 mikono mifupi ya heshima inayochomekwa kwenye sketi

- ❖ Viatu vya ngozi nyeusi vya kamba visiwe na visiginovirefu na si mabuti jozi mbili, visiwe nap ambo lolote.

- ❖ Trackasout ya michezo rangi ya Blue.

**MUHIMU**

1. Mwanafunzi aje na sweta lake rangi ya blue iliyoiva kwa ajili ya baridi
2. Mwanafunzi antakiwa awe na T-shirt moja rangi ya blue yenye nembo ya shule.
3. Sare itakayoshonwa tofauti na maelezo itapelekea mwanafunzi asipokelewe shuleni
4. Mwanafunzi aje na mchango wa BIMA YA AFYA YA JAMII TSHS. 5000/= ni muhimu sana kuwa na bima ya afya awepo shuleni.

**SAMBAMBA NA HAYO:-**

- ✓ Mwanafunzi atakayeenda kinyume na sheria za shule, basi ataadhibiwa vikali, ikiwemo kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule kabisa.
- ✓ Mwanafunzi anatakiwa aoneshe nidhamu, usafi na bidii katika masomo ili aweze kufikia malengo ya wizara katika viwango vya ufaulu vilivyowekwa na shule na Baraza la mitihani la Taifa.

**MWISHO**

Pamoja na barua hii naambatanisha na fomu nne A, B, C na D ambazo zitatakiwa zisomwe na zijazwe kikamilifu kabla ya mwanafunzi kuja Shuleni na baada ya kujazwa fomu zirudishwe shuleni yaani fomu B,C & D ambazo ni:-

b) Mambo binafsi ya mwanafunzi

c) Taarifa Binafsi za Mwanafunzi (medical examination) ijazwe na daktari wa serikali iwekwe na muhuri

d) Fomu ya kukiri na kukubari sheria za shule.

UONGOZI WA SHULE UNATEGEMEA USHIRIKIANO WA HALI YA JUU KUTOKA KWA MZAZI WA MWANAFUNZI, JUMUIYA, VIONGOZI WA SERIKALI, TAASISI, MASHIRIKA N.K KATIKA KUMLEA MWANAFUNZI NA KUWA NA MAADILI MAZURI NA BORA KWA MANUFAA YA JAMII NA TAIFA KWA UJUMLA .

**ELIMU BORA NI TOCHI YA JAMII**
**KARIBU SANA KINAGA SEKONDARI TUELIMIKE**
**KAULIMBIU YETU NI KIINGEREZA KWANZA.**

**…………………….**
**BUPILIPILI, J**
**MKUU WA SHULE**
**NAMBA YA SIMU. 0787882804**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia Sheria na taratibu zote za Shule kama zilivyoorodheshwa hapo chini.

1. **HESHIMA**
   - i. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
   - ii. Mwanafunzi hatakiwi kutumia lugha mbaya (matusi), wakati wowote kati yake mwenyewe na mwanafunzi wenzake, kwa walimu wake na watu wengine.
   - iii. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake
   - iv. mwanafunzi anatakiwa kuthamini, kuheshimu na aoneshe ushirikiano na kuSaidiana katika kazi zote akiwa shuleni.
   - v. Mwanafunzi harusiwi kuvta sigara, kufuga kucha ndefu, kuwa na nywele ndefu zikiwa chafu, kufuga ndevu, kuvaa mavazi yasiyo na heshima na kugombana.
   - vi. Mwanafunzi atatakiwa kuitika mara moja na kukimbilia aliko mkuu.
   - vii. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa, piacha za viongozi wa serikali nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na Fedha za nchi.
   - viii. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu ofisi za shule, mali ya binafsi na mali ya umma, mahali pa kulia chakula na ukumbi wa mikutano.
   - ix. Mwanafunzi anatakiwa kusimama kwenye mstari wakati wote wa kupokea huduma
   - x. Mwanafunzi anatakiwa kunyosha mkono juu na asimamame
   - xi. Mwanafunzi anatakiwa kuwa mfano wa kuigwa wakati wote mahali popote.
   - xii. Mwanafunzi anatakiwa kukaa kimya wakati wote anapokuwa darasani na aitoke nje bila ya ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyepo.
   - xiii. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu na kukubali tofauti za kisiasa, kidini na kiutamaduni zilizopo katika jamii na shuleni kwa ujumla.

2. **MAHUDHURIO**
   - i. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria shule muda wote wa masomo
   - ii. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria kazi zote za mikono
   - iii. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano ya shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya taifa n.k

3. **KUWAHI**
   - i. Mwanafunzi anatakiwa kudhamini muda
   - ii. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa.
   - iii. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi eneo husika naposikia wito wa dharura
   - iv. Mwanafunzi anatkiwa kufika shuleni ka tarehe zilizopangwa
   - v. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu kengele na kukimbia kuwahi kwenye paredi akisikia kengele.

4. **SARE ZA SHULE**
   - i. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare wakati wote akiwa darasani, nje ya shule katika BARAZA, anapokwenda Hospitali, katika maandamano na wakati wa kwenda na kurudi nyumbani.
   - ii. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa vazi la kazi wakati wa kazi tu
   - iii. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nguo za michezo wakati wa michezo tu
   - iv. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa kofia, viaatu vya ghorofaa na mapambo akiwa shuleni.

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.**

i. Wizi
ii. Uasherati, Ubakaji au Ushoga
iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
iv. Uvutaji bangi
v. Makosa ya jinai
vi. Kupigana au kupiga
vii. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
viii. Kudharau Bendera ya Taifa
ix. Kuoa au kuolewa
x. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
xi. Kutoa mimba
xii. Kukataa adhabu kwa makusudi
xiii. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu.

***NB: Soma kanuni na sheria hizi kwa umakini mkubwa na utakapokuwa shuleni utatakiwa kuzifuata zote bila kudharau hata moja. Kwa kuzingatia haya tutaifanya jamii ya Kinaga sekondari kuwa ni yenye kufuata maadili ya kitanzania.***

**SHULE YA SEKONDARI KINAGA**
**(PERSONAL PARTICULAR) FORM YA MAMBO BINAFSI**
**(IJAZWE KWA HERUFI KUBWA)**

**NYONGEZA B:**

1. Jina kamili …………………………………………….
2. Tarehe ya kuzaliwa……… mwezi …………. Mwaka ……………
3. Utaifa ……………………….. kabila ………………………………
4. (a). Anwani kamili ya nyumbani (yaani ya mzazi/ mlezi)
   ……………………………………………………..
   ……………………………………………………..

   (b). Wakati wote wa masomo taja mahali utakapokaa ……………………………..
5. a). Jina la Baba ……………………………………….. hai/ amefariki
   b). Kazi yake ………………………………………..
   c). Anuani yake ……………………………………….
   d). Namba ya simu …………………………………..
   e). Kama unatunzwa na mlenzi taja mahali anapoka ………………………………
6. a). Majina ya ndugu wa kiume
   i. …………………………………
   ii. ………………………………….

   b). Majina ya ndugu wa kike
   i. ……………………………………
   ii. …………………………………….
7. Mbali na masomo, mimi (mwanafunzi) ………………….. huwa napendela na kujishughulisha na michezo kama
   i. …………………………………………………………
   ii. …………………………………………………………..

Mimi Mzazi/Mlezi wa ……………………………………. Naahidi kumpa mahitaji yote ya shule kwa muda unaotakiwa.

Jina la mzazi/ Mlezi …………………………………………………….

Sahihi yake …………………………………. Tarehe ………………………

NYONGEZA C

## MEDICAL EXAMINATION FORM

KINAGA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 413,
KAHAMA.

**REF: FOR MEDICAL EXAMINATION**

This form must be completed by a government Medical Officer

- Student's full name: ……………………………… Present age ………………
- Blood Test …………………………………………
- Stool examination …………………………………
- T.S test ……………………………………………
- Asthma …………………………………………….
- Eye disorder ……………………………………..
- Skin disorder ……………………………………
- Anemia ……………………………………………
- Chest ……………………………………………..
- Operations ………………………………………
- Serious accident …………………………………
- Any other infections …………………………….
- Pregnancy ………………………………………. (in case of female)

**ADDITIONAL INFORMATION e.g physical defect of impairment, chronic family diseases e.t.c**

i. ……………………………………………………
ii. …………………………………………………..
iii. …………………………………………………..

I certify that I have personally examined Mr/ Miss …………………………….. and found him/her that he/she is fit/unfit for further studies at …………………… (Station).

Designation …………………………………………. (Official stamp)……………………

Station …………………………………………………….

**NYONEZA D:**

**FOMU YA KUKUBALI SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.**

Mimi ………………………………………………. (mwanafunzi) ninakiri kuwa nimezisona sheria na kanuni zote za shule ya sekondari Kinaga na kuzielewa, na kuwa nipo tayri kuzifuata na kuzitekeleza ilu kudumisha nidhamu na Taaluma katika Shule ya Sekonadari Kinaga.

Jina …………………………………… Sahihi ………………………. Tarehe ……………

NB. Fomu hii iletwe shuleni ikiwa imejazwa kikamilifu siku ya kuripoti shule.